# TUJIFUNZE BIBLIA

## *SOMO LA 2*

## AGANO LA KALE

Katika Biblia vimo vitabu 66. Vitabu hivi vimegawanyika katika sehemu mbili. Vitabu 39 vimo katika sehemu iitwayo **AGANO LA KALE** na vitabu vingine 27 vimo katika sehemu iitwayo **AGANO JIPYA**. Labda umefadhaika kujua kwa nini zimeitwa hivyo. Jibu ni kwamba katika Biblia twapata habari ya maagano makuu mawili yaliyofanywa kati ya Mungu na wanadamu. (Neno **"agano" maana yake ni mapatano** kati ya watu.) Kwa hiyo, sehemu ya kwanza ya Biblia huitwa **AGANO LA KALE** kwa sababu habari ya agano (au patano) la kwanza kati ya Mungu na watu inapatikana katika sehemu hii. Vile vile, sehemu ya mwisho ya Biblia huitwa **AGANO JIPYA** kwa sababu habari ya agano la pili kati ya Mungu na wanadamu inapatikana katika sehemu hii.

Ukizidi kutazama Biblia, utaona kwamba kila kitabu kimegawanyika katika milango (au sura) na mistari. Vitabu vimegawanyika katika milango na mistari ili iwe rahisi kupata kwa haraka maneno yo yote ya Biblia. Kazi hii ya kugawa vitabu haikufanywa na wale waandishi wa vitabu bali watu wengine waliifanya baadaye.

**Vitabu 39 vya Agano la Kale viliandikwa** kwa lugha ya **Kiebrania**. Baada ya miaka mingi vilitafsiriwa katika lugha ya Kiyunani, kisha vilitafsiriwa katika lugha za siku zetu. Katika vitabu hivi yamo mambo mengi sana yanayoweza kumfurahisha na kumpendeza msomaji wake. Twasikitika kwamba nafasi ya somo hili inatuwezesha kutaja kwa haraka tu mambo machache yaliyo muhimu zaidi katika kuelewa historia ya Agano la Kale.

Katika kitabu cha kwanza cha Biblia twasikia jinsi Mungu alivyoumba mbingu na nchi na vitu vyote vilivyomo. Mungu alipowaumba **ADAMU na HAWA** aliwakataza wasile matunda ya **mti wa ujuzi wa mema na mabaya** ili wasiadhibiwe. Adui ya Mungu, aitwaye **IBILISI au SHETANI**, aliwajia Adamu na Hawa katika mfano wa nyoka, akiwadanganya ili waivunje amri hiyo ya Mungu. Kuvunja amri ya Mungu ni dhambi ambayo hutenga watu mbali na Mungu na kuleta adhabu (Isaya 59:2). Mungu alisikitika sana kuona kwamba watu wake walijitenga mbali naye; lakini, alikuwa na mpango wa kuwasaidia wanadamu. Kwa hiyo, alisema kwamba uadui utakuwapo kati ya Shetani na uzao wa mwanamke na kwamba uzao wa mwanamke utaponda kichwa cha Shetani (Mwanzo 3:15). Katika maneno hayo Mungu alikuwa akitabiri kwamba, kutokana na uzao wa mwanamke, mtu fulani atazaliwa ambaye atamshinda shetani. Mtu huyo huitwa **MWOKOZI** na tutajifunza mambo mengi yanayomhusu tunapoendelea katika masomo yetu.

Adamu na Hawa waliwazaa **KAINI na HABILI**. Siku moja Kaini alimkasirikia Habili, akamwua. Kwa sababu ya dhambi hiyo Mungu hakutaka Mwokozi azaliwe kutokana na Kaini bali aliwapa Adamu na Hawa mtoto mwingine aitwaye **SETHI** (Mwanzo 4:25) Adamu na Hawa walizaa watoto wengine baada ya Sethi. Watu walipoanza kuwa wengi duniani walijawa na uovu kiasi cha kumfanya Mungu asikitike kwamba aliwaumba. Alikuwa na nia ya kuwaangamiza wote kwa maji ya gharika. Lakini mtu mmoja alipatikana aliyekuwa mwema. Mtu huyu alikuwa **NUHU**. Mungu alimwambia Nuhu kujenga **SAFINA** (chombo cha kuelea majini) ili aokoke. Katika safina iliyojengwa na Nuhu, Mungu aliokoa baadhi ya wanyama pamoja na watu wanane. Watu hao walikuwa Nuhu na mke wake pamoja na **SHEMU, HAMU, na YAFETHI**

(wana wa Nuhu) na wake zao. Kutokana na watu hawa dunia iliweza kujawa tena na wanadamu (Mwanzo 6-8). Baada ya gharika Mungu alimchagua Shemu ili mwokozi azaliwe kutokana naye.

Mtu mmojawapo wa ukoo wa Shemu alikuwa **ABRAMU**. Mungu alibadilisha jina lake Abramu liwe **IBRAHIMU** na alifanya agano pamoja naye. Katika agano hili, Mungu alimwahidi Ibrahimu kwamba atamfanya kuwa taifa kubwa na kuwapa uzao wake nchi ya **KANAANI**. (Kwa ajili ya ahadi hiyo, Kanaani huitwa "nchi ya ahadi".) Vile vile, Mungu alimwambia kwamba "*katika wewe jamaa zote za dunia watabarikiwa*" (Mwanzo 12:2-3; 17:1-11). Mungu aliposema kwamba jamaa zote za dunia watabarikiwa katika Ibrahimu alikuwa akionyesha kwamba Mwokozi atazaliwa kutokana na uzao wake. Ndiyo maana katika Biblia twasikia mambo mengi kuhusu taifa hili la Ibrahimu.

Wakati ule Mungu alipomwambia Ibrahimu kwamba taifa litatoka kwake, Ibrahimu hakuwa na mtoto. Tena, yeye pamoja na mke wake walikuwa wamezeeka sana. Walakini, Ibrahimu alimwamini Mungu na, kwa hiyo, Mungu aliwawezesha kumzaa mtoto **ISAKA**. Isaka aliwazaa Esau na Yakobo. Kati ya hawa, Mungu alimchagua **YAKOBO** ili taifa la Ibrahimu (pamoja na Mwokozi) litokane kwake. **Mungu alibadilisha jina la Yakobo liwe ISRAELI**. Israeli alikuwa baba ya watoto wa kiume 12. Makabila 12 ya Israeli yalitokana na wana hawa wa Israeli (Mwanzo 12-38).

YUSUFU alikuwa mtoto mmojawapo wa Yakobo (yaani, Israeli). Yusufu aliuzwa na ndugu zake awe mtumwa katika nchi ya Misri. Walakini, Mungu alimsaidia Yusufu na alipata kuwa mtu mkuu katika serikali ya Misri. Kwasababu hiyo, jamii yote ya Yakobo walihamia Misri (Mwanzo 37-50). Waisraeli hawa walikaa Misri miaka mingi sana wakiongezeka kuwa wengi mno. Baada ya kifo cha Yusufu, mfalme mwingine wa Misri aliwafanya Waisraeli kuwa watumwa. Mungu aliwasikia watu wake wakilia katika mateso yao na alimchagua **MUSA** ili awaongoze watoke katika Misri. Mungu alileta mapigo makali juu ya Wamisri ili mfalme wao, **FARAO**, awape Waisraeli uhuru (Kutoka 7-14). Walipotoka Misri Waisraeli waliingia jangwani. Hapo Mungu alifanya agano pamoja na Waisraeli akiahidi kuwabariki ikiwa watazishika amri zake.

Musa aliambiwa kupanda **mlima wa SINAI** na kupokea **TORATI** (au sheria) ili aipeleke kwa taifa la Waisraeli. (Sehemu mojawapo ya sheria hiyo huitwa **AMRI KUMI**.) Waisraeli waliambiwa kujenga **MASKANI** (hema) ya kumwabudia Mungu. Ndugu wa Musa, **HARUNI**, alichaguliwa pamoja na uzao wake ili wawe **MAKUHANI** wa Mungu (Kutoka 20-40). Haruni alikuwa mtu wa kabila la Lawi na kwa hiyo, makuhani wote pia walikuwa **WALAWI**. Makuhani hawa waliamriwa na Mungu kutoa sadaka na dhabihu za wanyama kwa ajili ya dhambi za Waisraeli. Dhabihu na sadaka hizo hazikuweza kuondoa kabisa dhambi. La! Bali tutajifunza jinsi dhambi zinavyoweza kuondolewa katika somo la tatu. Mambo mengi yanayohusu makuhani yanapatikana katika kitabu kiitwacho <u>Mambo ya Walawi</u>.

Katika vitabu vya <u>Hesabu</u> na <u>Kumbukumbu la Torati</u> twasikia jinsi Waisraeli walivyovunja amri za Mungu mara nyingi walipokuwa jangwani. Hata Musa mwenyewe alivunja amri mojawapo na, kwa hiyo, Mungu alimwambia kwamba atakufa bila kuingia katika nchi ya ahadi. Kabla ya kifo chake, Musa aliwakumbusha Waisraeli habari ya sheria na agano la Mungu. Katika agano hilo, Mungu aliahidi kuwapa nchi ya Kanaani na kuwabariki ikiwa watatimiliza wajibu wao katika agano. Wajibu wa Waisraeli katika agano ilikuwa kushika sheria za Mungu. Musa aliwaonya sana kwamba wakimsahau Mungu na kuvunja sheria zake basi baraka zote za Mungu pamoja na nchi ya Kanaani zitaondolewa kwao. Musa alipokufa Mungu alimchagua **YOSHUA** asimame mahali pa Musa na kuwaongoza Waisraeli. **Kitabu cha <u>Yoshua</u>** kinatuambia jinsi Waisraeli walivyoweza kupata nchi ya Kanaani.

Baada ya kifo cha Yoshua, Waisraeli walimsahau Mungu na walivunja sehemu yao katika agano. Hata ingawa walifanya hivyo, Mungu hakuwaondoa katika Kanaani mara bali aliwaadhibisha kwa kuleta adui

zao kuwatesa sana. Waisraeli walipotubu Mungu aliwainua watu fulani waitwao **WAAMUZI** ili waongoze Waisraeli na kuwasaidia kushinda adui zao. Habari za siku hizo zinapatikana katika **kitabu cha Waamuzi**.

Waisraeli walianza kutaka mfalme atawale juu yao ili wawe kama mataifa mengine. **SAULI** alikuwa mfalme wa kwanza wa Waisraeli. Mwanzoni Sauli alikuwa mtu mwema, lakini baadaye alimwasi Mungu. Kwa hiyo, Mungu alimchagua **DAUDI** kuwa mfalme badala ya Sauli. Mungu alipendezwa na Daudi kwa sababu alijitahidi sana ili ashike sheria zote za Mungu. Kwa kweli, Daudi alitenda dhambi. Walakini, alipotambua dhambi zake, hakusitasita bali alitubu mara akijaribu kuondoa uovu wake. Mungu alimwambia Daudi kwamba ufalme wake hautakoma kamwe (2Samweli 7:16). Hapo Mungu alikuwa akitabiri habari ya yule Mwokozi ya kwamba atakuwa mfalme wa milele kutokana na uzao wa Daudi.

**SULEMANI**, mwana wa Daudi, alikuwa mfalme wa tatu wa Waisraeli Mungu alimpa hekima na akili kupita watu wote (1Wafalme 4:29-34). Yeye aliandika vitabu vya Mithali, Mhubiri na Wimbo Ulio Bora. Sulemani alipokufa, Waisraeli wengi hawakutaka **REHOBOAMU** (mwana wa Sulemani) awe mfalme. Kwa hiyo ufalme uligawanyika; Rehoboamu alikuwa mfalme wa sehemu iitwayo **UFALME WA YUDA** na **YEROBOAMU** alikuwa mfalme wa sehemu iitwavo **UFALME WA ISRAELI**. Baada ya wafalme hawa, walikuwapo wafalme wengine wengi wa Yuda na wa Israeli pia. Habari za wafalme hao zinapatikana katika vitabu vya Samweli, Wafalme, na Mambo ya Nyakati.

Katika siku za wafalme hao, Mungu aliwatuma manabii wengi ili watabiri mambo yatakayotendeka baadaye. Katika Agano la Kale vimo vitabu 17 vilivyojawa na maneno ya unabii. Kwa hiyo, hatutaweza kusema sana kuhusu mambo yale yaliyotabiriwa bali tutataja mambo machache tu. Kwa mfano, manabii wengine walitabiri kwamba kwa ajili ya dhambi zao, watu wa ufalme wa Israeli watatekwa mateka na Waashuru na kwamba ufalme wa Israeli utaangamizwa kabisa. Jambo hili lilitendeka sawasawa kama lilivvotabiriwa. Manabii wengine walitabiri kwamba ufalme wa Yuda nao utatekwa mateka na Wababeli na kwamba, baadaye, baadhi ya Wayahudi hawa watarudi Kanaani. Jambo hili lilitendeka vile vile. Baadhi ya Wayahudi waliweza kurudi Kanaani kusudi Mungu atimize ahadi yake kwa Daudi jinsi alivyomwambia kwamba ufalme wake hautakoma kamwe. Hata ingawa Wayahudi walirudi katika nchi yao, lakini hawakuwa huru bali walikuwa chini ya mamlaka ya mataifa mengine. Walakini walikumbuka maneno ya manabii wengi waliotabiri kwamba mfalme atazaliwa kutokana na uzao wa Daudi ambaye atawaokoa watu wake. Kwa hiyo, walikuwa na hamu kubwa sana kumwona Mwokozi huyu.

Manabii wa Agano la Kale walitabiri mambo mengi ya ajabu kuhusu Mwokozi. Mungu aliwawezesha kufanya hivyo kusudi Waisraeli wawe tayari kumtambua na kumpokea Mwokozi atakapozaliwa. Miongoni mwa mambo yaliyotabiriwa ni haya: (1) Atakuwa wa ukoo wa Ibrahimu na Daudi, (2) atazaliwa katika mji wa Daudi (yaani, Bethlehemu), (3) atazaliwa na bikira, (4) atakuwa mfalme wa milele, (5) atawapoza wagonjwa, (7) atateswa kwa makosa yetu, (8) atasulibishwa pamoja na waovu, (9) watu watapiga kura kwa nguo zake, (10) damu yake itamwagika kwa ajili yetu, (11) mifupa yake haitavunjwa hata mmoja, (12) atazikwa pamoja na matajiri, (13) atafufuka bila kuona uharibifu, (14) atapaa kwa Mungu katika mawingu. Mambo mengi mengine yalitabiriwa ambayo hatutaweza kuyataja hapa. Basi katika somo la tatu tutaona jinsi mambo yale yaliyotabiriwa kuhusu Mwokozi yalivyotimilizwa katika maisha ya **YESU KRISTO**.

*************************************************************************************

***KANISA la KRISTO***

***Tanzania***

## *MASWALI*

Andika mstari chini ya jawabu lililo kweli kati ya majibu matatu yanayofuata kila swali.

1. Mtoto ambaye Mungu aliwapa Adamu na Hawa badala ya Habili alikuwa: Hamu - Sethi - Yusufu.
2. Mtu aliyejenga safina alikuwa: Yakobo - Musa - Nuhu.
3. Hesabu ya watu waliookolewa katika safina ilikuwa: 5 - 8 - 38.
4. Jina la Abramu lilibadilishwa liwe: Israeli - Isaka - Ibrahimu.
5. Jina la Yakobo lilibadilishwa liwe: Israeli - Isaka - Ibrahimu.
6. Yakobo alikuwa baba ya watoto wa kiume: 8 - 3 - 12.
7. Mfalme wa Misri alikuwa: Farao - Sauli - Sulemani.
8. Mtu aliyepokea sheria katika mlima Sinai alikuwa: Haruni - Musa - Daudi.
9. Mtu aliyechaguliwa badala ya Musa ili awaongoze Waisraeli waingie Kanaani alikuwa: Yusufu - Yafethi - Yoshua.
10. Mfalme aliyempendeza Mungu zaidi alikuwa: Sauli - Daudi - Farao.

Ikiwa maneno yafuatayo ni ya kweli uandike mstari chini ya neno "Kweli." Ikiwa maneno ni ya uongo, uandike mstari chini ya neno "Uongo."

1. Ibrahimu alikuwa kijana mwenye watoto wakati Mungu alipomwambia kwamba taifa litatoka kwake. Kweli Uongo
2. Mtu yule ambaye Mungu alisema kwamba atamshinda Shetani huitwa Mwokozi. Kweli Uongo
3. Watu wa ufalme wa Yuda huitwa Wayahudi. Kweli Uongo
4. Waisraeli hawakuvunja sehenu yao katika agano kati yao na Mungu. Kweli Uongo
5. Mungu alimpenda Daudi kwa sababu Daudi hakutenda dhambi yo yote. Kweli Uongo

Andika majibu kwa maswali yanayofuata.

1. Neno "agano" maana yake ni nini? __________________
2. Makabila 12 ya Israeli yalitokana kwa wana wa nani? __________________
3. Watu ambao walitumwa na Mungu ili watabiri mambo yatakayotendeka huitwa nani? __________________
4. Haruni alikuwa mtu wa kabila gani? __________________
5. Mfalme aliyekuwa na hekima na akili kupita watu wote alikuwa nani? __________________

**************************************************************************************

Baada ya kuyajibu maswali yote uandike jina lako na anwani yako na utume karatasi ya maswali kwa anwani iliyoandikwa hapa chini. Baada ya kuisahihisa tutairudisha kwako pamoja na somo jipya.

Jina lako ……………………………………………………

Anwani yako ……………………………………………

***KANISA la KRISTO***
***Tanzania***